# Uamili wa Ngazi ya Utambuzi katika Riwaya za Kiswahili

*Dinah Sungu Osango, Mwenda Mbatiah* na *Rayya Timammy*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Makala haya yanaangazia na kuchunguza dhana ya ngazi ya utambuzi na uamili wake katika riwaya za Kiswahili zilizoteuliwa makusudi kuukita na kuuendeleza mjadala unaodhamiriwa katika makala haya. Ngazi ya utambuzi ni mojawapo ya ngazi mbalimbali za ufokasi zilizopendekezwa na wananaratolojia kama vile Uspensky (1973) na Rimmon-Kenan (1983). Kimsingi, ufokasi ni mtazamo ambao huchukuliwa katika kuwasilisha simulizi na kuikuza hadithi tawala kwa ujumla. Ufokasi unajishughulisha kubaini ni nani anayeona kinachosimuliwa katika simulizi. Ufokasi ni istilahi iliyobuniwa na wananadharia ya naratolojia kurejelea kile ambacho katika uhakiki wa kijadi kilijulikana kama kitazamio. Abrams (1993) anaifafanua dhana hii ya ufokasi kuwa inarejelea jinsi hadithi inavyowasilishwa yaani, njia ambazo mwandishi anazitumia kusawiri na kuwasilisha kwa msomaji wahusika, dayalojia, matendo, mandhari na matukio yanayounda simulizi katika kazi ya bunilizi. Kwa upande wake, Hawthorn (2010:122) anasema kwamba, istilahi ya "kitazamio" haipambanui ni nani msemaji na nani anayeona na nini anachoona katika simulizi. Hii ndiyo sababu Genette (1972) alibuni istilahi hii ya ufokasi kama mkakati wa kuwezesha kutambua na kutofautisha kati ya msemaji na mfokasi katika simulizi za kifasihi. Kwa kujikita katika dhana hii ya ufokasi, msomaji au mchanganuzi anaweza kutambua pale ambapo mwandishi ndiye aliyeyashuhudia au anayeyashuhudia matukio au pale ambapo mwandishi anamtumia mmojawapo wa wahusika kuwasilisha ujumbe wake. Ili kutuwezesha kubainisha uamili wa ngazi ya utambuzi katika riwaya ya Kiswahili, data ya kuudhibiti na kuthibitisha madai ya mjadala tawala itatolewa katika riwaya za Kiswahili zilizoteuliwa makusudi zikijumuisha (C.S.L. Chachage, 2005), *Nyuso za Mwanamke* (S.A. Mohamed, 2010), *Harufu ya Mapera* (K. W. Wamitila, 2012), *Hujafa Hujaumbika* (F.M. Kagwa, 2018), *Haini* (Adam Shafi, 2002), na *Ndoto ya Almasi* (Ken Walibora, 2006). Uteuzi wa riwaya hizi unahalalishwa kwa misingi kwamba, hizi ni riwaya zilizo na matini pana zinazowezesha udondoaji wa mifano faafu inayodhihirisha ngazi za ufokasi na wakati huo huo kudhihirisha uamili wa ngazi hizo katika simulizi. Mjadala wa kimsingi katika makala haya umekitwa na kuongozwa na madai ya teneti za kimsingi za Nadharia ya Naratolojia ambayo inatambua ufokasi na uhusika kama vipengele muhimu katika uwasilishaji wa simulizi.**

**Maneno Muhimu**: *Ufokasi*, *Nadharia ya Naratorojia*, *Ngazi ya Utambuzi*, *Uamili*

**Utangulizi**

Ngazi ya utambuzi katika simulizi inahusisha hisi za binadamu zinazodhibitiwa na masafa ya wakati na masafa ya mahali kwa mkabala wa kinachosimuliwa (Rimmom-Kenan, 2003). Hisi hizo zinajumuisha usawiri na usanifu wa hisia za: kunusa, kusikia, kuonja, kuona, na kugusa kwa kadri zinavyosanifiwa kama sehemu au mkakati wa uwasilishaji kauli katika simulizi. Kwa mfano, dhana nzima ya kusikia kama kipengele cha masimulizi au mkakati wa usimulizi inahusiana na ubainikaji au ujitokezaji wa sauti, kelele, milio na usemaji katika simulizi. Kwa upande mwingine, mwono unahusiana na dhana ya kuona inayorejelea vitu au watu ambao wanaonekana, kuwa makini, kutoona au kuona kinachorejelewa na kuona kupitia kwa mtu mwingine. Nayo hisi ya mguso inajumuisha masuala yanayohusiana na uchungu, utambuzi wa kiwango cha nyuzi joto, pamoja na utambuzi wa nishati ya mwendo. Utambuzi wa hisi hizi katika simulizi, mara nyingi unahusishwa na uchanganuzi wa vipengele viwili muhimu ambavyo ni pamoja na utambuzi wa umbali au masafa ya mahali na masafa ya wakati. Masafa kati ya msimulizi na kile kinachosimuliwa huwa na athari changamano kuhusiana na maana ya ujumbe na maudhui yanayowasilishwa katika matini simulizi. Dhana ya masafa katika simulizi huwa na wasifu wa kujitokeza kwa njia mbili kuu, ujitokezaji kwa njia ya

usambamba wa upeo wa macho au ujitokezaji wima. Hii ina maana kwamba, mfokasi anaweza kuwa karibu na kile kinachosimuliwa au akawa katika masafa ya mbali na hicho kinachosimuliwa. Masafa haya yanaweza yakamwongoza msomaji katika kutambua mitazamo, misimamo na hisia za wahusika katika riwaya kwa upande mmoja na mwonoulimwengu wa mwandishi kwa upande mwingine.

Wakati unaotumiwa na msimulizi kuwasilisha ujumbe wake huwa na athari tata kwa ujumbe, hasa jinsi ujumbe huo utakavyopokelewa na utakavyofasiriwa na msomaji. Kupitia kwa utambuzi wa wakati uliotumika, msomaji anaweza kuvutwa karibu na ulimwengu wa hadithi au kujitenga na hadithi hiyo kutokana masafa ya umbali wa wakati. Wananaratolojia kama vile Genette (1980) na Rimmon-Kenan (2003) wanaainisha vipengele mbalimbali vinavyoweza kuchunguzwa katika kutambua na kutathmini masafa ya wakati. Vipengele hivyo ni pamoja na njeo, usahili au uchangamano wa mpangilio wa matukio, muda wa matukio, na uradidi wa matukio. Katika makala haya tumechunguza jinsi vipengele hivi vinavyofanikisha sio tu uwasilishaji wa ujumbe na dhamira za mwandishi bali pia, jinsi vinavyokuza wahusika katika riwaya mahususi.

**Msingi wa Nadharia**

Kama tulivyotanguliza, mjadala tawala wa makala haya unaongozwa na Nadharia ya Naratolojia. Nadharia ya Naratolojia ina misingi yake katika kipindi cha urasimi ambapo Plato na Aristotle walichangia katika kukuza Nadharia ya Simulizi (Gholami, 2013). Makala ya kwanza ambayo yanarejelea Nadharia ya Simulizi ni yale ya Plato katika kitabu chake cha *The Republic*. Katika kazi hiyo, Plato anaelezea na kuzifafanua istilahi mbili za kimsingi kuhusiana na usimulizi; dhana ya mimesia kwa maana kuwa, hadithi inasimuliwa moja kwa moja mbele ya hadhira. Dhana ya pili anayoifafanua Plato ni daijesia ili kukuza uelewa kwamba, msimulizi anaweza kuchangia katika usimulizi wa hadhira. Kwa upande mwingine, Aristotle anachangia zaidi ufafanuzi wa nadharia hii ya naratolojia katika *Poetics* anapoelezea maana ya tanzia. Anasema kuwa, ploti ya tanzia lazima iwe na mwanzo, kilele na mwisho. Maelezo yake kuhusu tanzia katika ushairi yalikuwa na mchango mkubwa katika kudhibiti uelewa wa naratolojia kwa kadri ilivyokuwa inakita misingi yake katika kipindi hicho.

Kuibuka kwa hadithi fupi na riwaya kama tanzu za fasihi katika karne ya 18 ambapo usimulizi ulijitokeza kwa mapana, kulishurutisha wananadharia wa baadaye kuanza kuiangalia upya na kutathmini Nadharia ya Simulizi. Nadharia ya Simulizi haikuwa na budi kufanyiwa marekebisho na mabadiliko ya kimsingi yaliyofikia kuibuka kwa Nadharia ya Naratolojia kama inavyoeleweka katika vipindi vya sasa. Wananaratolojia kama vile Roland Barthes (1966) Tzvetan Todorov (1968) na Algirdas Greimas (1973) waliamini kuwa palikuwa na haja ya kutunga sheria ambazo zingedhibiti simulizi ili kufanikisha uainishaji wa simulizi mbalimbali kwa kadri zilivyojitokeza katika riwaya, hadithi fupi, na bunilizi nyinginezo zilizokuwa na wasifu wa usimulizi. Wananaratolojia hawa wanaweza kuangaliwa kuwa ndio waliokuwa wa kwanza kuhusisha simulizi za kinathari katika hadithi na nadharia hii.

Kikundi kingine cha wananaratolojia kama vile Vladimir Propp (1968), Gérard Genette (1972) na Seymour Chatman (1978) kilifuata mtazamo wa kuchambua simulizi kwa kurejelea diskosi. Wananadharia hawa walijishughulisha kutunga sheria ambazo walizichukulia kuwa faafu kudhibiti simulizi katika riwaya kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Kwa mfano, Genette (1972) alichangia katika ukuzaji na uimarishaji wa Nadharia ya Naratolojia, hasa inapozingatiwa kwamba, Genette anatambulisha mambo matatu muhimu yanayoshurutisha kuzingatiwa katika simulizi. Kimsingi, mambo haya—yaani simulizi, hadithi na usimulizi ni uhalisia unaotegemeana, unaojengana na kujalizana. Kwa sababu ya kujibainisha kwa misingi iliyo na mahusiano ya karibu sana, Genette anapendekeza kutofautishwa kwa anayesimulia na anayeona matukio yanayosimuliwa katika simulizi. Kwa hivyo, anapendekeza istilahi ufokasi kama kipengele kinachomdhihirisha anayeona matukio na anayesimulia matukio. Mbali na haya, Genette anatambua aina tatu za ufokasi: ufokasi ndani, ufokasi nje na ufokasi nunge. Kuibuka kwa istilahi na dhana nzima ya ufokasi, kuliwachochea wananaratolojia wengine kufanya utafiti zaidi ili kutatua utata uliokuwapo hapo awali kuhusu tofauti kati ya anayesimulia hadithi na yule anayeona matukio.

**Mihimili ya Naratolojia**

Ushirikishwaji wa Nadharia ya Naratolojia katika makala haya, unaegemezwa katika mihimili ambayo iliwezesha kudhibiti hoja, kauli na mahitimisho yanayotolewa katika mjadala tawala wa makala haya. Awali, ufokasi ni mhimili muhimu unaotuwezesha kubaini kama anayeyaona matukio yuko ndani ya hadithi au anayatazama matukio kutoka nje ya hadithi. Kwa uelewa huo, hiki ni kipengele muhimu kinachowezesha utambuzi wa aina za ufokasi zinazojitokeza katika riwaya za Kiswahili.

Mhimili wa pili ni mhimili wa wakati unaotumiwa ili kuwezesha kuangaliwa na kuchunguzwa kwa vipengele viwili vikuu vya wakati ambavyo ni masafa ya mahali na masafa ya wakati. Masafa ya kisimulizi ni kipengele kinachotumiwa kubaini umbali kati ya msimulizi na masimulizi au kubaini maelezo yanayowasilishwa. Masafa hayo yanaweza kuwa mafupi au marefu. Kipengele cha wakati kinahusisha mpangilio, muda, marudio na mwendo. Wakati unatuwezesha kujua kipindi ambacho mhusika alijihusisha katika matukio ili kufahamu sifa zake kulingana na nyakati mbalimbali.

Mhimili wa tatu ni mhimili wa usimulizi, ambao ni muhimu katika kuwezesha kubaini na kutathmini masuala yanayohusiana na mawasiliano ya binadamu. Utambuzi wa usimulizi ni muhimu katika kuwezesha utambuzi wa aina mbalimbali za usimulizi kama mkakati wa kujenga uhusiano kati ya kile kinachosimuliwa na matumizi ya lugha.

Nne, naratolojia pia hutambua uhusika kama mhimili muhimu katika uchanganuzi wa simulizi katika riwaya. Sifa za wahusika zinaweza kubainishwa kutokana na maelezo ya msimulizi kuhusu tabia zao au kupitia kwa matendo, kauli za wahusika wengine, majina ya kimajazi au kupitia kwa mwonekano wao wa nje.

Mwisho, tumetumia mhimili wa uwasilishaji wa usemi na fikra kama kipengele cha kimsingi katika utambuzi na uchanganuzi wa simulizi. Usemi kama uwasilishaji wa maneno au sentensi kwa kadri zilivyosemwa na wahusika (Short 1991), unaweza kuwasilishwa kupitia kwa njia mbili kuu: usemi halisi au usemi wa taarifa.

**Njeo ya Kisimulizi**

Moja ya ngazi ya utambuzi ya kimsingi inahusiana na kipengele cha wakati ambacho hujitokeza kupitia kwa njeo mbalimbali zinazodhihirishwa kupitia kwa wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao. Simulizi inayosimuliwa katika wakati uliopo huonekana kana kwamba inasimuliwa wakati huo huo huku matukio yanapotukia. Hivyo basi, mkabala huu wa usimulizi humshirikisha msomaji na matukio hayo pamoja na wahusika wake kwa karibu. Kwa upande mwingine, simulizi inayosimuliwa katika wakati uliopita humfanya msimuliwa kuyaona matukio yanayosimuliwa kama ambayo yalitukia zamani au yalitendeka mbali naye, kwa hivyo, anaweza kuyatambua na kuyaelewa masimulizi pasina kujihusisha nayo kwa karibu. Kipengele cha njeo ni muhimu katika ngazi ya utambuzi kwa kuwa kupitia kwa nyakati mbalimbali, vipengele vingine vya ngazi ya utambuzi vinaweza kutambuliwa, kutathminiwa na kuchanganuliwa. Usimulizi katika riwaya za Kiswahili unaokitwa katika matumizi ya nyakati hizi ni uhalisia unaojitokeza kwa wingi ila wakati mwingi wasomaji hawatathmini uamili wa nyakati katika ukuzaji wa dhamira na uwasilishaji wa maana.

Matukio na utukiaji mwingi katika riwaya ya *Haini* yamesimuliwa pakubwa katika wakati uliopita, japo mara kwa mara msimulizi ametumia wakati uliopo hasa pale anapotaka kumleta msomaji karibu na matukio ya wahusika fulani au kumshirikisha msomaji katika matukio hayo. Kwa mfano, msimulizi-mfokasi ametumia nyakati tofauti kisanaa ili kudhihirisha kilichokuwa kikijiri mahakamani na wakati huohuo pia kuonyesha usuli wa matukio hayo yanayojitokeza mahakamani. Kwa mfano, anatumia wakati uliopita ili kuonyesha sababu ya ukumbi wa mahakama kujaa kama ifuatavyo:

> Washitakiwa peke yao walijaza ukumbi huo na safu tano za mbao zilipangwa kwa ajili yao. Walifika pale mahakamani kwa basi kubwa la polisi chini ya ulinzi wa kukata na shoka wa askari waliojizatiti, bunduki mkononi, mabomu ya machozi kiunoni, tayari kwa lolote litakalotokea… (uk. 230).

Baada ya kutumia wakati uliopita kusimulia jinsi washitakiwa walivyofikishwa mahakamani, msimulizi-mfokasi anabadilisha mkabala wa usimulizi na kutumia wakati uliopo ili kuonyesha jinsi wake wa washtakiwa hao walivyokuwa na hamu ya kuwaona waume zao kama ifuatavyo;

> Ndani, ukumbi wa mahakama umejaa hapana hata pa kutia mguu, nje, askari wanasukumana na watu wanaotaka kuingia kwa nguvu ndani ya ukumbi ule wa mahakama. Khadija yuko mbele anaongoza kundi kubwa la wanawake, wanasukumana na askari huku wakipiga kelele, "Tupisheni tukawaone waume zetu!" (uk. 231).

Msomaji anapoisoma sehemu hii anaweza kuona hali halisi ya mazingira haya kana kwamba yumo kwenye mahakama hiyo. Msimulizi-mfokasi anakamilisha masimulizi yake kuhusu jinsi washukiwa walivyokuwa wamekamilisha kujitetea kwenye mahakama hiyo na jinsi ilivyobainika kuwa mshukiwa mmoja alikuwa ameuawa akiwa katika seli. Jambo hili halikumfurahisha Chopra, kiongozi wa mashtaka kwa kuwa hakutarajia kifo cha mshukiwa huyu kutajwa na washukiwa. Msimulizi anatumia wakati uliopita kudhihirisha hasira ya Chopra ambayo inakuwa chanzo cha tabia yake baadaye kwenye mahakama hiyo. Anasema;

> Chopra alimtazama kwa hasira kubwa akainama chini na kutikisa kichwa. Taarifa ya daktari juu ya kifo cha Amhasi ilisomwa mbele ya mahakimu kama alivyoeleza Bwana Chopra kwamba alikufa kwa ugonjwa wa tumbo la kuhara (uk. 256).

Kutokana na tukio hilo, Chopra anaapa kuwaumbua washukiwa wakati wa kuwauliza maswali. Maswali yake yalilenga kuwadunisha na kuwachanganya hadi wajipate wamejitia kitanzi kwenye kesi zilizowakabilili. Msimulizi-mfokasi anapomtazama Chopra, anasimulia jinsi alivyojitayarisha kwa kutumia wakati uliopo kama ifuatavyo;

> Leo Chopra amevaa suti nyeusi na tai nyeusi. Siyo kwa sababu vazi hilo huvaliwa na mawakili wanapokuwa mahakamani bali kwa sababu ya kuwapa ishara washtakiwa kwamba msiba mkubwa unawasubiri, wao na walio wao wote. Kila mtu amekaa pale anamsubiri yeye atoe maelezo yake katika mahakama ile na hasa siku ile, siku inayosubiriwa na kila mtu. Amekaa pale juu ya kiti kwa kiburi na majivuno. Wote wale, maisha yao yamo mikononi mwake (uk. 258).

Matumizi ya wakati uliopo yanamruhusu msomaji kushuhudia hali ya wasiwasi inayowakumba washtakiwa huku Chopra akiwa na matumaini ya kuwashawishi majaji kuwa wale waliokuwa kizimbani walikuwa na hatia ya mauaji. Msimulizi anamdhihirisha Chopra kama mtu mwenye kiburi na majivuno anapoelezea jinsi alivyokuwa ameketi kwenye kiti pale mahakamani. Huenda kiburi hiki amekipata kutokana na tajriba yake ya kuzitumikia serikali mbalimbali. Tabia yake ya kuwa kigeugeu inadhihirika wakati msimulizi-mfokasi anaposema kuwa hapo awali alikuwa ameifanyia kazi serikali ya Malkia Elizabeth wa Pili, kisha akamfanyia kazi Sultani na wafuasi wake, na sasa alikuwa ameaminiwa na uongozi wa Kigogo kama mwanasheria mkuu. Chini ya tawala mbalimbali, ameifanya kazi yake kwa uaminifu wa uongozi tofauti. Kwa mfano, licha ya kufanyia kazi serikali ya Malkia Elizabeth, baada ya mkoloni kuondolewa alikuwa mstari wa mbele kuutetea uongozi wa Mwafrika. Kwa hivyo, msimulizi-mfokasi anatumia nyakati mbili ili kulingalisha mabadiliko katika maisha ya wahusika kama vile Chopra.

**Mpangilio**

Kipengele kingine cha utambuzi ambacho ni muhimu katika kutambua usimulizi na uwasilishaji wa mambo mbalimbali katika riwaya, ni mpangilio na mfuatano wa matukio katika hadithi kulingana na jinsi yalivyowasilishwa katika simulizi. Hadithi hujibainisha kutokana na mpangilio wa matukio kiwakati. Hata hivyo, mkondo asilia wa matukio unaweza kukiukwa kwa kutumia mbinu kama vile analepsia na prolepsia (Propp, 1968, Bal 1985). Katika hali hii simulizi huruka matukio kadhaa na kwenda mbele hatua fulani au kurudi nyuma hatua fulani lakini bado kunadumishwa mantiki ya jinsi matukio haya yanyovyohusiana. Anelepsia ni mbinu ya kisimulizi inayotokea wakati ambapo

mpangilio wa hadithi kikronolojia unakiukwa ili kutoa masimulizi ya matukio ya hapo awali, yaliyotokea kabla ya matukio ya sasa yanayosimuliwa katika simulizi husika (Genette, 1980). Mwandishi anatumia mkabala wa kumrudisha msomaji wake nyuma kwenye matukio yaliyofanyika wakati uliopita ili kutoa usuli wa tukio linalosimuliwa kwa sasa kwa kuangazia mambo yaliyotokea kabla ya tukio hilo na jinsi mambo hayo yanavyohusiana na ya sasa.

Katika riwaya ya *Harufu ya Mapera*, mwandishi ametumia mbinu ya anelepsia katika sehemu nyingi ili kumwelekeza na kumbainishia msomaji juu ya maisha ya awali ya wahusika kama vile Pipo Kenya na Jude Kinya. Kwa mfano, kupitia anelepsia, tunafahamishwa kuhusu maisha ya wazazi wa Jude Kinya. Jude anamweleza mwanawe, Jimna jinsi babake alivyokuwa na uwezo mkubwa huko mashambani lakini pia, alikuwa na chuki fulani kwa watu maskini. Jude anaendelea kumsimulia mwanawe jinsi babake alivyokuwa mchoyo kwa maskini kiasi kwamba, hata ilikuwa muhali kuwapa maskini chochote wakati wa shida. Ilikuwa ni kawaida yake kuwasuta na kuwakejeli maskini ambao walifika kwake kuomba. Mfano ufuatao unadhihirisha jinsi babake Jude alivyokuwa amemtusi mwanamume mmoja maskini kwa sababu ya kuomba chakula. Jude anasema:

> ... Jinsi alivyomzomea na kumkashifu kwa kuwa mwanamume mzima mwenye ndevu, jitu lisilokuwa na haya ambalo badala ya kulima kwa bidii lilijihangaikia kwa watu limebeba mkebe kusaka msaada… Akamuuliza kwa nini alikuwa na mikono miwili, miguu miwili, macho mawili… Hivi hakuweza kutumia akili yake na kujitoa kwenye joko la dhiki alikotumbukia au kwa maneno ya babake, alikoamua kujitosa kama nondo mjinga… (uk.149).

Kupitia kwa mkabala huu wa kisimulizi wa anelepsia, wasomaji wanafahamishwa asili ya Jude Kinya. Kinya alizaliwa na kulelewa katika familia tajiri iliyojitambulisha kwa kushabikia utabaka, familia ambayo, kwa maoni na imani za babake, watu walikuwa maskini kwa sababu ya kujinasibisha na kuushabikia uzembe, ujinga na tabia ya kupenda kuombaomba. Msimamo huu haukumpendeza Jude, na ndiyo sababu alifanya uamuzi kisiri wa kumwauni mzee huyo aliyefika kwao kuomba chakula. Jude aliingia kwenye ghala la chakula na kuchota makopo kadhaa ya mahindi na kuyapitishia kwenye dirisha ili kumkabidhi huyo mwanamume aliyekuwa na njaa. Tukio hili linadhihirisha misimamo tofauti kati ya baba na mwanawe. Babake Jude alikuwa mfano wa matajiri ambao huwachukulia maskini kuwa watu wajinga na ambao wamejitakia hali yao hiyo kutokana na ujinga wao wa kutotaka kufanya kazi kwa bidii. Kwa upande mwingine, Jude anadhihirisha msimamo tofauti na ule wa babake tangu utotoni kwani, yeye anaonyesha utu kwa watu maskini. Hili linadhihirika pia katika maisha yake ya baadaye anapojitolea kwa vyovyote vile kuwasaidia watoto mayatima waliokuwa katika makaazi ya watoto yatima ya Jumba la Malezi. Aidha, hii ndiyo sababu anamsimulia mwanawe kisa hiki ili kumtahadharisha dhidi ya tabia hii ya utabaka.

Katika *Harufu ya Mapera*, prolepsia imetumiwa kumdokezea msomaji jinsi Isabelle angekuja kujuta baada ya kumwambia Caliban siri yake ya kutokuwa na ujauzito wa Jimna. Hapo awali, Isabelle alikuwa amemwambia Caliban kuhusu hiyo siri yake. Lakini kwa sababu Caliban alikuwa ndumakuwili, alikuwa amemweleza Jimna siri hiyo ili kujikombakomba kwake. Kwa kuwa Isabelle hakutarajia siri yake kutambulika hasa na Jimna, anaapa kumwadhibu Caliban. Hata hivyo, msimulizi-mfokasi anadokezea kuwa mambo hayangemwendea vyema Isabelle kama alivyotarajia kama ilivyo katika dondoo hili:

> ... Isabelle akakiuma kidomo chake. Huyo Caliban atamtambua. Kwa nini ameamua kuifichua siri ambayo alimwomba asiifichue? …Aliapa kimoyomoyo kuwa atahakikisha kuwa amepata funzo lake. Laiti angejua kuwa alikuwa anaatika mbegu za jambo ambalo atalijutia baadaye (uk. 485).

Isabelle alipokutana na Caliban, alimdhalilisha kwelikweli, akamtusi na kumfedhehesha sana. Kutokana na fedheha hiyo, Caliban naye anaapa kumpa mwenzake funzo la maisha. Zamu yake ya kulipiza kisasi iliwadia wakati Isabelle alipotaka msaada kutoka kwake ili kumwadhibu Jimna aliyekuwa amemkasirisha. Wawili hawa walikubaliana kukutana ili kupanga jinsi shughuli yao ingetimizwa. Kabla ya kukutana kwao, msimulizi-mfokasi tena anamdokezea msomaji kuwa mambo

yangemwendea mrama Isabelle wakati anaposema, "Laiti angejua kuwa alikuwa anajiingiza kwenye jiriwa..." (uk. 546).

Caliban aliichukulia nafasi hii kama fursa yake ya kulipiza kisasi, kwa hivyo, anapanga na mwandishi mmoja wa habari kuyarekodi matukio ambayo yangetokea wakati angekutana na Isabelle. Walipokutana, Caliban alikuwa amemnunulia chakleti ambayo alimkabidhi kwa njia ya kimapenzi. Mazungumzo yake yote kwa Isabelle yalidhihirisha kuwa alikuwa mpenzi wake. Wakati haya yote yanapoendelea, mpiga picha alikuwa akiifanya kazi yake ya kuchukua picha kama alivyokuwa amepangiwa na Caliban. Wakati huohuo, Caliban alimtumia Jimna ujumbe kupitia kwa nambari isiyojulikana. Ujumbe ulimjulisha kuwa Isabelle alikuwa kwenye mkahawa wa Turtle Doves na ujumbe ulimtaka aende huko. Jimna aliamua kwenda huko ambako alimpata Isabelle akiwa mezani huku akinywa kinywaji. Kando yake kulikuwa na gilasi nyingine ambayo Jimna alishuku ilikuwa ya rafikiye Isabelle. Wakati hayo yakijiri, Caliban alikuwa ametokomea, lakini alikuwa ametimiza kisasi chake cha kuwakosanisha wawili hawa.

Kwa upande mwingine, prolepsia ni mbinu ya usimulizi ambapo msimulizi anasimulia matukio ya hadithi, yatakayotokea baadaye kabla ya muda wake kufika. Msimulizi huangazia matukio ambayo hayajatokea kama anavyosema Rimmon-Kenan (1983), kuwa mbinu hii hupeleka simulizi katika matukio ya baadaye. Hivyo basi, mbinu hii humwezesha msomaji kutambua mambo yatakayomtendekea mhusika kabla ya mhusika mwenyewe kujua. Kwa mfano, katika *Nyuso za Mwanamke*, msimulizi-mfokasi anaeleza kuwa Bi. Mau alitabiri kurejea kwa kitukuu chake:

> … Au nani aliyethubutu kushuku uwezo wake wa kutabiri yasiyotabirika? Kwani si ameshatabiri mengi kwa usahihi kabisa? Mara ngapi hapo nyuma yeye alikwisha tambua kuwa siku moja kitukuu chake kingerejea kuishi kwao licha ya Bw. Hila kukizuia kisikaribie nyumbani humo… (uk. 174).

Aidha, Bi. Mau anatabiri kuwa huyo Nana ndiye angeleta matumaini katika nyumba yao. Haya yanakuja kutimia baadaye kwani Nana alitoroka kwao huku akimfuata Faisal ambaye anamwelekeza kwa nyumba ya Bi. Mau. Akiwa huko anaelekezwa na Faisal jinsi ya kukitumia kipawa chake cha uimbaji ili kujikimu. Kutokana na pesa alizozipata, Nana anawekeza katika biashara mbalimbali ambazo zilinawiri sana. Hili lilimsaidia sana kuisaidia familia yao, hasa Bi. Mau, katika mahitaji yake ya kila siku.

Kupitia kwa ufokasi nje, msimulizi katika *Makuadi wa Soko Huria* anamdokezea msomaji kuhusu maisha ya baadaye ya Mjuba na Sifuni. Haya yanatokea baada ya Bi. Mkubwa kutabiri kuwapo kwa uhusiano wa kimapenzi kati ya Mjuba na Sifuni baada ya kujumuika nao kwa muda mfupi. Wawili hawa walikuwa wakihusiana kikazi lakini hawakujua kuwa wakati mmoja wangekuwa wapenzi. Ila wanapokutana na Bi. Mkubwa, anawaambia kuwa wangekuja kuwa wapenzi na hata kuibariki ndoa yao. Anawaambia:

> "Na ninyi wawili: mshukuruni huyo aliyevumbua mapenzi kama kitu tunu. Nimewaangalia sana jioni ya leo. Mwenyezi Mungu awabariki mje kuishi maisha mema, na wanenu wajaliwe maisha bora zaidi kuliko haya tuliyoishi sisi." (uk. 252).

Utabiri wa Bi. Mkubwa ulikuja kutimia baadaye kwani Sifuni na Mjuba walijipata wakiwa wapenzi. Licha ya kuwa mwanzoni kulikuwa na shauku kuhusu uhusiano wao, wawili hawa walikuja kukubaliana kuwa walikuwa wanajaribu kulipinga jambo ambalo halingelipingika.

**Uradidi**

Mbinu nyingine inayotumika katika ngazi ya utambuzi ni mbinu ya uradidi ambayo hujishughulisha kuangalia na kuangazia ni mara ngapi tukio limetokea katika hadithi na katika matini simulizi (Genette 1980, Rimmon-Kenan 1983). Tukio linaweza kutokea mara moja lakini likasimuliwa zaidi ya mara moja, vinginevyo tukio linaweza kutokea zaidi ya mara moja lakini likasimuliwa tu mara moja. Kinachohitajika kuangaziwa hapa ni kwamba, kuna hali ambapo usimulizi wa matukio unarudiwarudiwa kwa njia za moja kwa moja au njia zisizo wazi, ambapo lengo la urudiaji huu linaweza kuwa ni kusisitiza ujumbe fulani, kukashifu kitendo fulani au kuonyesha mtazamo wa

msimulizi kuhusu tukio husika. Genette (1980) anaainisha aina tatu za uradidi zinazojumuisha; usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu. Katika usimulizi mosi, tukio linatokea mara moja na kusimuliwa mara moja. Usimulizi rudufu ni hali ambapo tukio linatokea mara moja lakini linasimuliwa mara kadhaa katika simulizi. Nao usimulizi banifu hutokea wakati ambapo tukio linatokea mara kadhaa lakini likasimuliwa mara moja.

**Usimulizi Rudufu**

Katika *Haini*, msimulizi-mfokasi anatilia mkazo maneno ya Kanali Bunju kwa Hamza kwa kuyasimulia mara mbili ili kudhihirisha athari yake kwa Hamza. Maneno hayo yalisemwa baada ya Hamza kupitishwa katika madhila na mateso ya hali ya juu akiwa mikononi mwa makanali ambao walikuwa wamempiga na kumwacha katika hali mahututi. Lengo la makanali hawa lilikuwa kumlazimisha kukubali kuwa alikuwa miongoni mwa mahaini waliokuwa wamemuua Kigogo. Licha ya kuwa Hamza anafanyiwa ukatili wa hali ya juu na hata kutishiwa kuuawa kwa kuwekewa bastola kichwani, anakataa kata kata kukubali kuhusika katika mauaji hayo. Kanali Bunju anakasirishwa na msimamo wa Hamza wa kutokubali kuhusika katika mauaji. Anasimama akiwa na bastola yake tayari kumuua Hamza. Makanali wenzake wanamshika na kumtuliza. Lakini, anatoa kauli ya mwisho iliyolenga kumtisha Hamza.Anamwambia,“Tunakupeleka chumba cha kiza. Tutakapokutoa huko uwe umeshaamua kimojawapo. Kukubali tulivyokwambia au kifo!” (uk. 84).

Athari ya maneno hayo inaonekana baada ya Hamza kufikishwa kwenye chumba hicho. Maneno hayo yanajitokeza tena katika mawazo ya Hamza. Tunajulishwa maneno hayo kupitia kwa msimulizi-mfokasi ambaye anaweza kuyasoma mawazo ya Hamza anapoyakumbuka moja kwa moja. Hamza anapatwa na udhia anapoyakumbuka maneno hayo kwa kuwa yanamkumbusha ukatili wa makanali wakiongozwa na Kanali Bunju. Hili ni baada ya yeye kukumbana na hali halisi ya chumba cha kiza, chumba kilichokuwa sawa na jahanamu.

Katika *Ndoto ya Almasi*, ukatili wa mzee Masasi wa kumwadhibu mkewe unasisitizwa kwa kusimuliwa mara kadhaa. Kisa hiki kimesimuliwa mara ya kwanza wakati ambapo Almasi anayakumbuka masaibu yaliyompata dadake, Nakhumicha baada ya kuringwa. Babake alimpiga Nakhumicha kama mnyama (uk. 21). Aidha, kisa hiki kinasimuliwa tena wakati kunatokea ugomvi kati ya mzee Masasi na mwanawe Almasi, kuhusu redio. Hili ni baada ya Masasi kuitaka redio yake ambayo ilikuwa imeharibika hapo awali lakini ikatengenezwa na Almasi ambaye kwa wakati huo alikuwa anaitumia. Mwanzoni, Almasi alikataa kumpa babake redio hiyo, kwa sababu kulingana naye, yeye ndiye alikuwa mmiliki kwa kuwa ndiye alikuwa ameikarabati. Babake alipoyasikia madai ya Almasi, anarudi nyumbani kwake kwa hasira. Hili linamfanya mamake kuhofia hatari hasa baada ya kukumbuka tukio moja lililokuwa limetokea hapo awali. Kupitia kwa ufokasi nje, msimulizi mfokasi anasema:

> ... Mama alikumbuka siku mumewe alipogundua binti yao Nakhumicha amepata mimba nje ya ndoa. Alimtandika bintiye nusura kumwua. Hata hatua ya mwenyewe Paulina binti Nikasio kujitia kati haikutosha. Baba mtu alimgeukia mama na kumtandika sawia na mtoto pasi huruma. Kama si Magdelina kumwahi mumewe Daktari Makabila na kumsihi kuingilia kati ... (uk. 80).

Baada ya kumbukumbu hiyo, mamake Almasi, alitahadhari kwa kumtafutia Almasi nauli ili aondoke katika boma lao kabla ya mumewe kumwadhibu. Tukio hili linadhihirisha itikadi ya Kiafrika pale ambapo mtoto akikosa pia mama huwa amekosa kwa kutomwelekeza mwanawe ipasavyo. Pia, sifa ya ukatili wa Masasi inadhihirika wakati anapompiga mwanawe na mkewe bila kujali iwapo wawili hao wangeyapoteza maisha yao au la.

**Usimulizi Banifu**

Baadhi ya matukio katika simulizi yanaweza yakafokasiwa mara nyingi lakini yakasimuliwa mara moja. Licha ya kuwa usimulizi huwa umebanwa, mitazamo na maana iliyokuwa imekusudiwa kuwasilishwa huwasilishwa. Aina hii ya usimulizi inaitwa usimulizi banifu. Katika *Nyuso za*

*Mwanamke*, tukio la babake Nana kwenda katika chumba cha Nana ili kumrai kutojifungia ndani, linatendeka mara nyingi lakini linasimuliwa mara moja. Kwa mfano, mfokasi-mhusika anasema:

> ... Sasa namwona baba yangu akifungua mlango wa chumbani kwake na kuandama ujia... Na mara hii, nyuma anafuata mama'ngu wa kambo. Baba amefanya hivyo mara milioni moja tokea asubuhi. Alitoka chumbani kwake kuelekea kwangu! Hufanya hivyo siku zote kwa hakika, pale ninapokuwa siwezi kuzizuia hisia na hasira zangu... (kur. 21-22).

Nana hujipata mara kwa mara akiwa amejifungia ndani ya chumba chake kutokana na mizozo ya mara kwa mara baina yake na babake, Bwana Hila. Chanzo cha mizozo hiyo kilikuwa ni utengano wa wazazi wake. Inasemekana kuwa babake ndiye aliyesababisha kutengana kwake na mkewe kutokana na dhuluma alizomfanyia mkewe. Kinachomuudhi zaidi Nana ni kuwa, babake hutaka kumlazimisha kuwa na uhusiano wa karibu na mamake wa kambo. Kwa kuwa Bwana Hila anafahamu kuwa yeye ndiye chanzo cha shida za Nana, huwa na wasiwasi sana ndiposa mara kwa mara hutoka chumbani mwake na kuelekea chumbani mwa Nana ili kumshawishi asikasirike.

**Usimulizi Mosi**

Katika aina hii ya usimulizi, tukio lililofokasiwa mara moja husimuliwa mara moja na msimulizi ambaye anaweza kuwa msimulizi-mfokasi au mhusika-mfokasi. Waandishi hutumia aina hii ya usimulizi hasa wanapotaka tu kutaja baadhi ya matukio ambayo hayafai kutiliwa mkazo sana au yawezayo kuuelekeza usimulizi kwengine kinyume na malengo ya msimulizi. Kwa mfano, katika *Haini*, maisha ya ujana ya Hamza yamesimuliwa tu mara moja mwanzoni mwa riwaya (uk. 1). Msimulizi-mfokasi anasema kuwa hapo awali Hamza alikuwa kijana aliyependa starehe sana. Mara kadhaa alikuwa amefumaniwa na mchumba wake akiwa na makahaba katika nyumba yake. Aidha, anasema kuwa mara nyingi alikuwa amepatikana njiani akiwa na wasichana huku amelewa chopi. Lakini baada ya usimulizi huu, msimulizi anarejelea hali ya sasa ya maisha ya Hamza hasa baada ya yeye kuoa na kutulia. Lengo la mwandishi lilikuwa kusimulia kuhusu maisha yake ya sasa wala si yale ya awali.

**Muda wa Matukio**

Dhana ya muda kama kipengele cha ngazi ya utambuzi hurejelea uhusiano ulioko kati ya tukio linalosimuliwa na wakati unaotumika kuliwasilisha au kulisimulia tukio hilo katika hadithi, simulizi au matini mahususi ya kifasihi (Rimmon-Kenan, 2003). Muda unaochukuliwa na tukio linalosimuliwa katika simulizi mahususi unaweza kuwa mrefu au mfupi. Ili kuutambua muda unaochukuliwa katika usimulizi huo, mchanganuzi anafaa kuchunguza wakati-hadithi na wakati-matini (Genette, 1980). Wakati-hadithi hurejelea muda ambao hadithi huchukua kuanzia mwanzo hadi mwisho ilhali wakati-matini hurejelea muda unaochukuliwa na msomaji kukamilisha kusoma hadithi fulani. Hata hivyo, kuna ugumu wa kukadiria muda unaochukuliwa na msomaji kumaliza kusoma hadithi kwa kuwa wasomaji mbalimbali wana uwezo tofauti wa kusoma na kuelewa hadithi. Toolan (2001) anapendekeza matumizi ya istilahi kama vile kasi na mwendo ili kupimia viwango mbalimbali vya muda. Naye Genette (1980) anapendekeza vipengele vinne vinavyofaa kuchunguzwa kama msingi wa kutambua muda na maana changamano zinazoweza kuhusishwa na muda. Vipengele hivyo ni pamoja na: mtuo, muhtasari, onyesho na udondoshi. Katika makala haya, ni muhimu kuangazia kipengele cha muda kwa kuwa ni kigezo cha msingi katika kuchunguza muda ambao mhusika amechukua katika kusimulia hali, tukio au tajriba fulani kwa uelewa kwamba, muda unachangia kubainisha sifa, tabia au uelewa wa masuala yanayowasilishwa.

Katika usimulizi, mtuo ni hali ambapo usimulizi wa hadithi husitishwa ili kuyapisha masimulizi mengine ambayo ni ya ziada. Wamitila (2008) anasema kuwa mtuo ni maelezo au mawazo ya ziada yanayotumika ili kusisitiza jambo fulani. Matumizi ya mtuo hufanya wakati wa kusimulia hadithi kuwa mfupi ukilinganishwa na wakati unaotumika kuelezea matini. Kwa hivyo, mbinu hii humfanya msomaji kutumia muda mrefu kuisoma hadithi ilhali hadithi yenyewe huwa imetua kwa kuwa msimulizi mara nyingi humrejesha msomaji katika matukio ya hapo awali au huyasimulia matukio ya ziada yanayoegemezwa kwenye hadithi kuu. Kwa mfano, katika *Nyuso za Mwanamke,* msimulizi-

mfokasi alipokuwa akisimulia kisa cha sherehe ya kuzaliwa kwake, anatua kuiendeleza hadithi hiyo ya sherehe za kuzaliwa kwake anapoamua kuanza kusimulia usuli wa jumba lao na jinsi babake alivyokuwa amelimiliki jumba hili na shamba lake kubwa. Usimulizi wake unaenda sambamba na upeo wa macho yake hadi kwenye jumba lao:

> ... Mara hii nadhari yangu ikanichukua na kunilazimisha kutazama (hata sijui kwa nini) lile jumba letu.
>
> Jumba letu lilikuwa pandikizi la jumba, kama vile limeshushwa kwa miujiza au kwa mbinu na fahari za uchawini. Ingawa likimeremeta mataa ya rangi mbalimbali, kwangu mimi leo lilitisha…. Taa ziliwaka kwa fujo wakati kwenye vitongoji vya karibu na hapo kulikuwa na giza tupu… (uk. 35).

Usimulizi huu unaendelea kwa kurasa kadhaa zinazofuata. Kupitia kwa mtuo na usimulizi huu, tunafahamishwa jinsi babake alivyolipata shamba lake kwa njia za kifisadi. Aidha, tumewezeshwa kutambua umbo na sura, na ukubwa wa jumba lenyewe unaosimuliwa kwa kina. Hapa tunapata mtazamo wa Nana kuhusu tabia ya babake. Kwa maelezo yake Nana, babake alikuwa dhalimu na mwenye ubadhirifu wa hali ya juu, wasifu ambao ulimfanya Nana kutofurahishwa na malalamishi ya wakulima waliokuwa wamenyang'anywa mashamba na babake. Baada ya kayasimulia haya, anamrejesha msomaji kwenye hadithi anaposimulia jinsi sherehe ilivyoendelea siku hiyo hadi ikafikia wakati ambapo aliamua kutoroka kwao.

**Muhtasari**

Usimulizi wa matukio na tajriba mbalimbali katika riwaya kama kazi za kubuni, hutumia mbinu pamoja na ufundi wa muhtasari kama njia ya kuharakisha hadithi. Licha ya kwamba mbinu hii ya muhtasari ina wasifu wa kuharakisha kasi ya uwasilishaji hadithi, lakini uharakishaji huo hautatizi wala kukinza ukuzwaji wa wahusika wa kutambua mambo kwa njia moja au nyingine. Muhtasari hutokea pale ambapo matukio fulani katika hadithi husimuliwa kwa ufupi. Hali hii inadhihirika katika *Hujafa Hujaumbika* wakati ambapo msimulizi-mhusika anatoa muhtasari wa maisha yake akiwa katika shule ya msingi;

> Huko Majengo Primary School, niliendelea vizuri kimasomo. Sasa nilikuwa katika mwaka wa kuiaga shule ya msingi. Shida kuu niliyokuwa nayo ilikuwa kurudi nyumbani mara kwa mara kwa kukosa ada kidogo tuliyotozwa ya masomo. Si mama pekee aliyeshindwa kunilipia karo. Wako wazazi wengi wengine waliokosa hata chakula na mavazi sembuse karo? ... (uk. 101).

Aya hii inadhihirisha ukakamavu na bidii ya Mwanga akiwa katika shule moja pale katika mtaa wa mabanda. Aidha, inatoa muhtasari wa maisha na changamoto alizopitia baada ya yeye na familia yake kuhamia katika mtaa wa mabanda. Lengo la msimulizi hapa lilikuwa kuonyesha mabadiliko yaliyotokea baada ya mamake kufutwa kazi. Licha ya kuwapo kwa changamoto hizo zote, Mwanga alivumilia na kujitahidi katika masomo yake. Kimsingi, mwandishi anataka kumfahamisha msomaji kuwa mitaa mingi ya mabanda hukumbwa na changamoto nyingi, lakini muhimu zaidi ni kuwa baadhi ya vijana hujikakamua na kufaulu maishani kama alivyofanya Mwanga.

Katika *Makuadi wa Soko Huria*, maisha ya awali ya Oscar yamesimuliwa kwa ufupi ili kuonyesha tabia yake kabla ya kuokoka. Hapo awali alikuwa mtu mpenda raha na aliyetenda dhambi nyingi. Oscar anasema kuwa kabla ya kuokoka kwake alikuwa sawa na Sauli wa Biblia kisha Bwana akamtoa kwenye vitendo vya dhambi alivyokuwa akivifanya. Kupitia kwa ushuhuda wake, msomaji anafahamishwa jinsi alivyokuwa na tamaa ya wanawake hadi akamringa Sifuni na kumwacha bila kuyajali maisha yake. Hili lilitokea sawia na kumringa msichana mmoja wa Kiislamu ambaye alikuwa bintiye waziri. Kutokana na tamaa yake ya mali, aliamua kumwoa binti huyo na kumwacha Sifuni aliyekuwa mchumba wake. Hata hivyo, hangeweza kuizuia tamaa yake kwa sababu wakati mmoja alisahau kuwa alikuwa amesilimishwa kwa hivyo akajipata akila nyama ya nguruwe iliyokuwa mwiko katika dini ya Kiislamu. Hiki kikawa chanzo cha kuzomewa na mkwe wake. Mwishowe, akaamua kurudi kwao. Baada ya kuhangaika akitafuta kazi kwa kipindi kirefu, akajipata akijihusisha na

walokole. Hali hii inamwezesha msomaji kutambua sababu za baadhi ya watu kubadilisha imani zao za kidini na sehemu za kuabudu mara kwa mara. Mara nyingi huwa wanaongozwa na tamaa ya kufaidika kutokana na madhehebu mbalimbali.

**Onyesho**

Dhana ya onyesho kama mbinu ya usimulizi, ni mkakati wa usimulizi ambapo mwandishi huwapa wahusika-wafokasi fursa ya kuwasilisha matukio moja kwa moja kadri yanavyoendelea kutukia. Rimmon-Kenan (2003) anasema kuwa, aina hii ya usimulizi huwaruhusu wahusika kudhihirisha hisia na mitazamo yao juu ya mambo, hali na tajriba za aina mbalimbali. Katika uhalisi wa onyesho, waandishi wengi hutumia usemi halisi au dayalojia ili kuwasilisha maneno ya moja kwa moja ya wahusika. Ushirikishaji wa wafokasi katika matukio husaidia kuyafupisha masafa ya wakati na masafa ya kiujumi yaliyopo kati ya mhusika na msomaji (Genette 1980). Masafa hayo yanapofupishwa, inakuwa rahisi kwa wasomaji kujitambulisha na kujihusisha na wahusika wa hadithi kwa matumaini kwamba, mitazamo yao itabainika na kukubalika na wasomaji kwa urahisi. Katika aina hii ya usimulizi, muda wa matini huwa sawa na muda wa hadithi. Kwa mfano, katika *Ndoto ya Almasi*, mazungumzo kati ya Chebosio na Almasi yanadhihirisha dharau ya Chebosio kama ifuatavyo:

> "Umekuwa kama baba lako?"
>
> "Ehe?"
>
> "Uliambie litoke kwetu. Ndugu zangu wakitoka Mombasa wakalipata litaona cha mtema kuni".
>
> "Aisee dharau kama hii haifai Chebosio."
>
> "Kwani wewe ni mtu wa kustahiwa? Umekuwa tangu lini? Nikome kama ulivyokoma la mamako." (uk. 52).

Chebosio anadhihirisha dharau kwa mwanamume aliyekuwa amehamia nyumbani kwa mamake baada ya kifo cha babake. Anatumia hali ya ukubwa anaposema, "Uliambie litoke kwetu." Kwake Chebosio, mwanamume huyo ni jitu lisilokuwa na akili wala faida yoyote. Licha ya kuwa alifaa kumheshimu mwanamume huyu kwa kuwa alikuwa mpenzi wa mamake, anadhihirisha dharau kubwa kwake. Aidha, anadhihirisha sifa ya kutojali hisia za watu wengine kwa kuwa huyo mwanamume aliyekuwa akizungumziwa alikuwa babake Almasi, ambaye alikuwa anazungumza naye kwa wakati huo. Alipokuwa akimkejeli babake Almasi, hakujali hisia zake. Kwa upande mwingine, Almasi anaonyesha tabia ya ukomavu na utulivu kwa kuwa hakuonyesha hasira zake kwa Chebosio hata baada ya yeye kumtusi babake.

Mwandishi wa *Hujafa Hujaumbika* anatumia mtindo wa kidrama ili kudhihirisha ulimbukeni wa wahusika kuhusu suala la UKIMWI kama ifuatavyo:

> Bunzi: … (*Kwa makini kama anayelevuka*) Lakini kaka, wewe unaamini kuna hili gonjwa linaloogopewa na kutangazwa kote kote kama nini? Kama lipo, mbona sisi hatujashikwa? … Na kama lingekuwako, mbona gonjwa lenyewe linatuogopa?
> Gunzi: Kama UKIMWI upo, huwashika waoga! (kur. 90-91).

Wawili hawa wanayaendeleza maisha yao ya ukahaba bila kujali kwa kuwa walikuwa na imani kuwa hakukuwa na ugonjwa wa UKIMWI. Kwa bahati mbaya wanapokumbana na ukweli wa mambo, walikuwa wamekwishaambukizwa ugonjwa huo na walikuwa katika hali mahututi. Wahusika hawa wanakuzwa kama watu wenye mapuuza, kwani licha ya serikali kuwahamasisha kuhusu athari za UKIMWI, wao hawatilii maanani mawaidha hayo. Hivyo basi, mwandishi anawajuza wasomaji jinsi ugonjwa huu umekuwa ukisambaa na kuenea licha ya serikali kuweka mikakati ya kukabiliana na janga hili.

**Masafa ya Mahali**

Masafa ya mahali hurejelea mahali alipo mfokasi wakati wa kusimulia hadithi. Masafa haya yanaweza yakawa ya karibu au ya mbali. Masafa haya hudokezea utambuzi wa mhusika kuhusu masuala mbalimbali yanayomhusu yeye au wahusika wengine. Mfokasi anaweza akawa mahali ambapo anayafuatilia matukio mengi ya hadithi ama akawa ndani ya hadithi huku akishiriki katika

matukio. Aina ya kwanza hutumika sana katika hadithi ambazo msimulizi huwa pia mfokasi. Nayo aina ya pili hupatikana katika simulizi zilizo na wafokasi ambao pia ni wahusika. Masafa haya pia huwaelekeza wasomaji kupata ujumbe uliokusudiwa kwa kuwa yanawezesha maana zilizokusudiwa kufasiriwa.

Waandishi wa riwaya tulizoziteua wametumia masafa ya mbali ili kusimulia tabia na sifa za wahusika. Kwa mfano, masafa ya mbali katika *Ndoto ya Almasi* yanampa nafasi nzuri mfokasi kuwaona wahusika watatu huku akisimulia hali zao kama ifuatavyo:

> … Almasi alimtazama dadake Naliaka aliyekuwa amekaa nje ya nyumba yake anaongoa kitoto alichokipakata. Kilikuwa uchi, haikuwa taabu kwa Almasi kugundua kuwa mpwa wake alikuwa kitoto kivulana. Kilikuwa kinalia mtawalia, bila kukoma. Macho yao yalipokutana Naliaka aliinuka mara moja na kumpiga pambaja nduguye. Hapo ndipo Almasi alipogundua kuwa Naliaka alikuwa na kitoto kingine tumboni. Dada mtu alionekana kazeeka kuliko umri wake hasa. Alikuwa amevaa gauni la bluu. Gauni lenyewe limechanika kifuani kuyadhihirisha waziwazi maziwa na chuchu zake (uk. 81).

Almasi anapomwona dadake, anatambua jinsi maisha ya kimaskini yalivyokuwa yamemdhuru. Kutokana na mavazi yake yaliyokuwa yameraruka, Almasi alitambua kuwa dadake alikuwa akiyaishi maisha magumu mno. Hali hii ndiyo inayomfanya kuonekana mzee zaidi kuliko umri wake. Aidha, Almasi anatambua kuwa dadake alikuwa mja mzito licha ya kuwa alikuwa na mtoto mwengine mchanga. Suala la kuwapata watoto wengi kuliko uwezo wa kiuchumi alionao mja linadhihirika kupitia kwa mhusika huyu.

Ngazi ya utambuzi inaweza kudhihirishwa pia kutokana na ufokasi wa masafa ya karibu. Katika aina hii ya ufokasi, matukio husimuliwa wakati huohuo yanapotokea. Msimulizi huwa ni mmoja wa wahusika anayeshuhudia au anayeshiriki katika matukio ya hadithi, kwa hivyo, hutambulika kama mhusika-mfokasi. Kwa kawaida mfokasi huyu ana uwezo wa kuyatambua tu yale matukio ambayo anaweza kuyaona. Katika *Hujafa Hujaumbika*, masafa ya umbali wa mahali yanapunguzwa wakati Mwanga anasimulia kisa kinachohusu sherehe za ndoa. Mwanga anasimulia yale anayoyaona na kila hatua ya sherehe hiyo. Sherehe hii inathibitisha kuwa katika jamii husika, mwanamke anastahili kuwa bikira kabla ya kuolewa. Hali hii inatokea kuwa kinyume, kwani katika arusi anayoishuhudia, msichana hakuwa bikira. Jambo hili linaiaibisha sana familia yake. Ila Mwanga, anaikemea jamii inayomsuta mwanamke, huku waliotia doa (wanaume) wakikosa kuchukuliwa hatua yoyote. Kwa mfano anasema:

> Mwanzo sikuelewa yaliyokuwa yakiendelea hasa iliposemwa, 'Harusi haikujibu'. Niliposaili nilifahamishwa kuwa mwari… hakuwa bikira kama alivyopaswa kuwa… Wasiwasi wangu ulikuwa kwamba ni mwanamke pekee aliyefaa kuudumisha ubikira wake! Nani alijali usafi wa mwanamume? (kur. 113-114).

Kulingana na Mwanga, suala la ubikira linafaa kuwahusu pia wanaume wala si wanawake pekee. Anapinga utamaduni ambao unaonekana kuegemea upande mmoja. Katika aina hii ya utamaduni, mwanamke ambaye anajihusisha kimapenzi na mwanamume kabla ya ndoa hupachikwa majina kama vile: kahaba, hawara, kiruka njia na mzinzi. Kwa upande mwingine, mwanamume anayejihusisha na wanawake wengi hukuzwa kwa kuitwa: mwanamume kwelikweli, hodari au mshindi (uk. 114).

**Matumizi ya Viashiria Kuonyesha Masafa ya Mahali**

Masafa ya ufokasi yanaweza pia kudhihirika kupitia kwa matumizi ya viwakilishi vya mahali. Viwakilishi vionyeshi hutumika ili kuashiria kitu kinachorejelewa kwa kutaja masafa yaliyoko baina yake na msemaji. Viashiria hivi hurejelea masafa ya karibu, wastani na mbali sana. Mifano ya viashiria ambavyo hutumika ni kama vile: huyu, huyo, yule, hapa, hapo, pale, hiki, hicho na kile miongoni mwa vingine vingi. Viashiria hivi vinapotumiwa katika simulizi, hutufahamisha jinsi wahusika mbalimbali wanavyotambua vitu, hali au mambo tofauti tofauti katika wakati fulani wa

maisha yao. Kwa mintarafu hii, msimulizi katika *Hujafa Hujaumbika* anatumia viwakilishi vya umbali na ukaribu kwa pamoja ili kuonyesha jinsi wanaume kutoka katika matabaka mbalimbali na wenye umri tofauti tofauti walivyoingia na kutoka chumbani mwa kahaba mmoja, Guguta baada ya kujifurahisha kimapenzi. Kahaba huyu hakujali umri wala fasili ya wanaume walioingia kwake mradi tu walikuwa na pesa. Shughuli za kuingia na kutoka nyumbani humo zinasimuliwa na msimulizi-mfokasi anaposema, "Mara kwa mara niliwaona wanaume wakipishana mlangoni mwa chumba chake mfano wa nyuki mzingani- huyu akiingia, yule anatoka..." (uk. 85).

Viwakilishi "huyu" na "yule" vimetumiwa ili kuwakilisha wanaume waliotoka sehemu mbalimbali ili kuja kumtembelea Guguta. Kiwakilishi cha ukaribu "huyu" kinasimamia wanaume waliotoka katika mtaa wa mabanda ambako aliishi kahaba huyo. Wanaume hawa ni kama vile Bunzi na Gunzi ambao walionea fahari kushindana na watu wenye vyeo katika kumfurahisha kahaba huyo. Nacho kiwakilishi "yule" kimetumiwa kuwakilisha wanaume waliotoka katika tabaka la juu ambao hawakujali hatari ya kujihusisha kimapenzi na kahaba huyo, licha ya kufahamu vyema hatari iliyokuwa inawakodolea macho. Kutokana na muktadha huu, tunaweza kutambua sifa za Guguta kama mwenye tamaa na mtovu wa nidhamu kwa kuwa hakujali wala kubaini ni nani aliyejihusisha naye kimapenzi. Matendo yake yalitawaliwa na tamaa ya kupata pesa.

**Hitimisho**

Makala haya yamejadili ngazi ya utambuzi kama inavyodhihirika katika riwaya teule za Kiswahili. Imebainika kwamba, ngazi hii ni muhimu katika uwasilishaji wa simulizi kwa kuwa inamwezesha msomaji kutambua masafa yaliyopo baina ya mfokasi na kile kinachofokasiwa. Masafa haya yanaweza kuwa ya mahali ama ya wakati. Wanaowasilisha simulizi wana jukumu la kuamua jinsi matukio na mitazamo ya wahusika itakavyodhihirika kwa wasomaji. Uteuzi wa kile kitakachofokasiwa na kile kitakachosimuliwa hutoa nafasi bora ya ufasiri wa ujumbe. Masafa ya mahali na wakati yametumiwa na watunzi wa riwaya teule ili kuzipa simulizi maana, kutoa mitazamo na hisia mbalimbali za wahusika. Masafa ya karibu, ya wakati na yale ya mahali yameyafanya matukio kuonekana kana kwamba yanatokea karibu na msomaji, hivyo basi kumpa fursa ya kujinasibisha na hisia na tajiriba za wahusika katika simulizi. Kinyume chake kinatokea iwapo masafa yaliyotumika katika simulizi ni ya mbali. Umbali wa kimasafa huyafanya matukio kuonekana kana kwamba yalitukia kitambo au mbali sana na msomaji hivyo basi uwezo wa kujihusisha nayo huwa mdogo ikilinganishwa na masafa ya karibu. Waandishi wa riwaya teule wametumia vipengele vya ufokasi kama vile: nyakati, mpangilio, muda na viashiria mbalimbali ili kufanikisha uwasilishaji wa uhusika na ujumbe uliokusudiwa.

**Marejeleo**


Abrams, M. H. (1993). *A Glossary of Literary Terms.* New York: Holt, Rinehart and Winston.

Bal, M. (1985). *Narratology. Introduction to the Theory of Narrative*. Toronto: University of Toronto Press. Toleo la 3 (2009).

Barthes, R. (1966). *Introduction to the Structural Analysis of Narratives*. Cambridge: University Press.

Chachage, S. C. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es Salaam: E&D Limited.

Chafe, W. (1994). *Discourse, Consciousness, and Time*. Chicago: University of Chicago Press.

Chatman, S. (1978). *Story and Discource: Narrative Structure in Fiction and Film*. Ithaca: Cornell University Press.

Fowler, R. (1966). *Essays on Style and Language: Linguistic and Critical Approaches to Literary Style*. London: Routledge and Kegan Paul.

________ (1986). *Linguistic Criticism.* Oxford: Oxford University Press.

Genette, G. (1972). *Narratology*. Imesomwa (Jumamosi 1/07/2017).

http://www.signosemio.com/genette/narratology.asp

__________ (1980). *Narrative Discourse*: *An Essay in Method.* Ithaca: Cornell University Press.

Gholami, V. (2013). "Conrad and Narrative Theory: A Narratological Reading of Selected Novels of Joseph Conrad". Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha London. Haijachapishwa.

Greimas, A. J. (1973). *On Meaning*. Minnesota: University of Minnesota Press.

Herman, L. na Vervaeck, B. (2007). *Handbook of Narrative Analysis*. London: University of Nebraska Press.

Kagwa, F. M. (2018). *Hujafa Hujaumbika*. Nairobi: Longhorn.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Propp, V. (1968). *Morphology of the Folktale*. Austin: University of Texas Press.

Ricoeur, P. (1981). *Narrative Time*. Katika W.J.T. Mitchell (ed.), On Narrative. Chicago: The University of Chicago Press.

Rimmon-Kenan, S. ([1983] 2003). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Routledge.

Shafi, A. S. (2003). *Haini*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Short, M. (1991). *Speech Presentation, the Novel and the Press. The Taming of the Text: Explorations in Language, Literature and Culture*. London: Routledge.

Todorov. T. (1990). *Genres in Discourse*. New York: Cambridge Press.

Toolan, M. J. (2001). *Narrative: A Critical Linguistic Introduction*. London: Routledge.

Uspenky, B. (1973). *A Poetics of Composition*. Berkeley and Los Angeles: University of California Press.

Walibora, K. (2006), *Ndoto ya* Almasi. Nairobi: Moran Publishers.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

___________ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.

___________ (2012). *Harufu ya Mapera*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.